# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Pili – Tarehe 12 Disemba, 2022.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma Nam. 1 ya 2007 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma Nam. 1 ya 2007 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

68. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kuzisaidia kaya masikini kila mwezi kwa kuwapa angalau Shilingi Elfu Ishirini (Tsh. 20,000/=), fedha ambazo japo hazisaidii mahitaji ya familia hizo lakini "kupata si kukosa" na moja shika sio kumi nenda uje.

(a) Je, ni kigezo gani kinachotumika mpaka kaya husika ikapata huduma hiyo ya kifedha.

(b) Kwa kuwa kuna manung'uniko makubwa ya watu wengi wasiojiweza kukosa huduma hiyo, ni lini Serikali kupitia sheria itafanya uhakiki mpya, ili wale wenye sifa za kunufaika na huduma hiyo waweze kupata fedha hizo.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

107. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ilipendekezwa na kuahidiwa na Serikali kwamba kutakuwepo vyombo huru vya kusimamia haki za binaadamu na Utawala Bora Zanzibar, ili kuweza kurudisha heshima na ulinzi wa haki za binaadamu na usimamizi wa Utawala Bora. Hata hivyo, hakuna juhudi makhsusi katika jambo hili.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali yetu inaridhishwa na hali ya sasa ya mwenendo wa Haki za Binaadamu na Utawala Bora Zanzibar.

(b) Je, tokea kumalizika kwa uchaguzi wa mwaka 2020, ni zipi juhudi za Serikali katika kuimarisha misingi ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora Zanzibar.

119. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR HASSAN (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Suala la utelekezaji wa wanawake na watoto limekuwa jambo la kawaida kwa jamii zetu, pamoja na ukweli kuwa, jambo hilo hupelekea athari nyingi kwa wanawake na watoto ikiwemo kukosa elimu, kutumia madawa ya kulevya na kupata maambukizi ya ukimwi.

(a) Je, ni lini sheria italitilia maanani suala hili.

(b) Je, kwa nini Serikali haiweki sheria maalum kwa akina baba wanaosaliti familia zao ambao hawako katika mfumo wa Utumishi Serikalini.

(c) Je, Serikali kupitia Mahakama ya Kadhi ina mpango gani wa kisheria kwa baba wanaotoa talaka kiholela na kupelekea kutelekeza familia zao.

<u>**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**</u>

98. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ Limited) iliwastaafisha wafanyakazi wake wasiopungua 118 kwa hoja ya kuibinafsisha Benki hiyo, jambo ambalo hadi leo halikufanyika na badala yake waliajiriwa wafanyakazi wengine wenye sifa zisizo bora kuliko wale waliostaafishwa. Aidha, zoezi hilo lilifanywa kinyume na Sheria ya Kazi na utaratibu halali kama ilivyoamuliwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania mwezi Agosti, 2021.

(a) Je, ni kwa nini hadi sasa Serikali haijatekeleza amri ya Mahakama kuhusiana na kesi hii.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kinadaiwa na wafanyakazi hawa kwa vile kinaongezeka kadiri Serikali inavyochelewesha kuwalipa.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwarejesha kazini wafanyakazi hao ambao Mahakama tayari zimetoa hukumu za kuamuru kurejeshwa huko.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

136. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya ukarabati wa soko la Darajani.

(a) Je, wafanyabiashara waliokuwa wakiuza wamepelekwa wapi.

(b) Baada ya kumalizika soko hili, Je, hatma ya wafanyabiashara hao itakuwaje.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

56. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuliimarisha Baraza letu la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), ingawaje bado linakabiliwa na changamoto mbali mbali za kutekeleza majukumu yake.

Je, ni lini Serikali italipatia BAKIZA jengo jipya la kufanyia kazi linaloendana na mahitaji yake ya sasa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

59. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Msitu wa kichunjuu uliopo katika Jimbo la Mtambile ni msitu muhimu sana ambao una vivutio vingi kwa Watalii wanaotembelea msitu huo kuangalia rasilimali zilizomo ndani yake wakiwemo popo.

(a) Je, msitu huo umeingizwa na umo katika hifadhi ya Taifa.

(b) Kama haumo, Je, mapato yake yanaenda wapi.

118. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali yetu imetumia gharama kubwa katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuandaa miundombinu pamoja na kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo hicho.

Je, kwanini hadi sasa kilimo cha umwagiliaji maji hakijaanza kutumika ipasavyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

17. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika eneo liliopo Skuli ya 'High Performance' katika jimbo la Mwanakwerekwe, limekuwa na changamoto ya muda mrefu sasa ya kupata umeme mdogo, hali ambayo sio tu inawaathiri wananchi wa eneo hilo, lakini pia ni hatari kwa mali zao hasa zinazotumia umeme.

(a) Je, nini chanzo cha tatizo hilo.

(b) Kwa nini tatizo hili limekuwa la muda mrefu sasa.

(c) Je, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), linaahidi tatizo hili litamaliza lini

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

8. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa muda mrefu sasa, kumejitokeza sintofahamu kubwa kwa wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe, kuhusiana na utambuzi wa maeneo ya wazi katika jimbo hilo.

(a) Je, Wizara yako imechukua juhudi gani kuondosha sintofahamu hiyo.

(b) Je, ni lini Wizara hii itayatambua maeneo yote ya wazi katika jimbo la Mwanakwerekwe, ili kuondoa utata na hatari ya uvamizi wa maeneo hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

32. MHESHIMIWA ABDULLA HUSSEIN KOMBO (Jimbo la Mkoani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali iliipeleka meli ya MV. Maendeleo chelezoni Mombasa kwa nia ya kuiboresha, ili irudi Zanzibar kuendelea kutoa huduma iliyokusudiwa ya usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

(a) Je, kabla ya meli hii kupelekwa chelezoni na baada ya kutengenezwa ilikuwa na thamani ya kiasi gani.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kuitengeneza meli hiyo.

(c) Je, ni kweli kuwa meli hiyo tayari imeshauzwa, na imeuzwa kwa kiasi gani cha fedha.

**Wizara ya Afya:**

26. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wananchi wa Shehia ya Kinowe wanaipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuwakubalia ombi lao la kujenga kituo cha Afya. Kwa kuwa ujenzi huo umeshaanza ambapo kwasasa upo katika hatua za kozi ya tano (5).

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hawa, ili waweze kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

(b) Je, Wizara inawaahidi nini wananchi hawa juu ya upatikanaji wa vifaa tiba na wataalamu watoa huduma za afya baada ya kukamilika kwa ujenzi huu.

93. MHESHIMIWA SABIHA FILFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Viongozi na wananchi wa Ndijani Mseweni wamejenga nyumba ya daktari karibu na kituo chao cha Afya, lakini wameshindwa kumaliza ujenzi wa nyumba hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi kumaliza ujenzi wa nyumba hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

137. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa kuwapatia mikopo wanafunzi wanaoingia katika vyuo vikuu hapa nchini.

Je, ulipaji wa mikopo hiyo ukoje kisheria kwa wanafunzi wanaomaliza masomo yao na bado hawajapata ajira.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

45. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Miongoni mwa kazi zinazohitaji uzalendo na uadilifu pamoja na kuipenda nchi yako, ni pamoja na uhifadhi na utunzaji wa vitu vya kale.

(a) Je, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale inawapatia posho la kutunza hazina hizi zenye thamani kubwa wafanyakazi wanaohusika na jukumu hili kubwa ili kuzidi kuwatia nguvu.

(b) Je, Idara inaendeleza utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwaendeleza wafanyakazi hao kwa lengo la kukuza ufanisi katika uwajibikaji wao.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

97. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kuna malalamiko ya msingi kutoka kwa wafanyakazi wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ambao walistaafishwa kinyume na utaratibu na Sheria za Kazi ambazo bado zinawatambua kama wafanyakazi. Hata hivyo, madai yao hayajashughulikiwa na Serikali kwa kutochukua hatua stahili ili kuumaliza utata wa suala hilo ikiwemo kuwalipa wahusika stahiki zao na kuwastaafisha kwa mujibu wa Sheria na taratibu.

(a) Je, ni upi ufafanuzi wa ZSTC kwa wafanyakazi waliostaafishwa, kwa Sheria na utaratibu upi.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwapatia haki zao na kuwarejesha kazini wafanyakazi wote wa ZSTC waliostaafishwa kinyume na utaratibu wa Sheria.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma Nam. 1 ya 2007 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Zanzibar,**
**12 Disemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**